

VIDOKEZO MUHIMU KWA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA UMEME



Matumizi mazuri ya huduma ya umeme yanaweza kuokoa fedha ambazo zingepotea kwa kulipia gharama zisizo na sababu za matumizi ya huduma hiyo.

Umeme wa ndani ya nyumba

- Tumia taa zinazoakisi mwanga kuliko taa za joto kali. Taa zinazoakisi mwanga ni bora zaidi na hudumu kiasi cha mara 4 hadi 10 zaidi.
 - Ingawa taa zinazoakisi ni ghali zaidi ya taa za joto kali, lakini zenyewe huokoa nishati kwa muda wote wa matumizi yake.
- Unapoweka mtandao wa nyaya (wiring) kwenye nyumba yako, hakikisha kuwa kazi hiyo inafanywa na fundi aliyesajiliwa na mwenye leseni ya EWURA
- Nyoosha nguo nyingi kwa wakati mmoja kuepuka uwashaji wa pasi wa mara kwa mara ili kuepuka kutumia kuwa kufanya hivyo unatumia uniti nyingi.
 - Nyoosha nguo nzito kwanza, kisha maliza na nguo nyepesi. Nguo nzito hutumia umeme mwingi, ilhali nguo nyepesi zinaweza kunyooshwa kwa kutumia joto la pasi lililopatikana ya kunyoosha nguo nzito.
 - Zima pasi mara unapotaka kufanya shughuli nyingine ili kuepusha nishati kupotea ovyo.
 - Zima pasi dakika tano kabla ya kumaliza nguo zote kwani pasi inakuwa bado na moto wa kutosha kumaliza nguo zilizobaki.
 - Ondoa pasi kwenye soketi ya umeme mara baada ya kumaliza kunyoosha nguo.
- Zima vifaa vyote vya umeme baada ya matumizi na uhakikishe umezima na kwenye soketi. Kutokuzima soketi kunaweza kusababisha umeme kuendelea kutumika bila ufahamu wako
- Kama hakuna ulazima wa vyakula au vinywaji kuhifadhiwa kwa ubaridi wa jokofu/friji, unashauriwa kutotumia friji yako
 - Pia usiweke Jokofu sehemu yenye joto kubwa au sehemu isiyo na mzunguko mzuri wa hewa kwani itatumia umeme mwingi.
 - Hakikisha ujazo wa Jokofu lako hauzidi robo tatu (¾) ya ujazo wake kwa ajili ya matumizi mazuri ya nishati.
 - Tumia jokofu lisilo chakavu kwani chakavu hutumia umeme mwingi.
 - Muda wote mlango wa jokofu uwe umefungwa ili kutunza baridi
- Usiunganishe vifaa vingi kwenye kebo ("extension") moja ya umeme kwa kuwa ikizidiwa uwezo wake, unaweza kusababisha majanga ya moto ama uharibifu wa vifaa vyako



- Usiwashe taa wakati wa mchana, tumia mwanga wa jua
 - Zima taa katika chumba chochote ambacho hukitumii
 - Tumia taa kwa matumizi katika eneo husika tu badala ya taa zenye nuru kali chumba chote, elekeza mwanga pale unapohitaji.
 - Tumia taa za njia zaidi za moja ili kurahisisha kupunguza kiwango cha mwanga wakati taa za nuru kali zinapo kuwa si za lazima.
 - Tumia taa zinazoakisi kiasi kidogo za wati za umeme au taa za usiku zinazong'aa.
- Pamba nyumba yako kwa rangi yenye kuakisi mwanga na pia fungua pazia ili kuruhusu mwanga wa mchana kupenya ndani
 - Weka madirisha makubwa unapojenga nyumba kuruhusu mwanga kuingia ndani wakati wa mchana badala ya kuwasha umeme kutwa nzima
- Safisha kuta za nyumba, taa na mifuniko yake ili kuondoa vumbi uweze kupata mwanga ulio sahihi na wa kutosha
- Tumia vifaa vya kurekebisha au kupunguza nguvu za umeme katika nyumba yako ili kuepuka hasara ya kuunguliwa na vifaa katika nyumba yako
- Ni rahisi kuchemsha maji katika birika kuliko katika jiko la umeme kwani jiko la umeme linachukua muda mwingi.
- Usitumie vifaa kama runinga, radio n.k kwa pamoja kwani vinaongeza matumizi ya umeme.

Umeme wa nje ya nyumba

- Wamiliki wengi wa nyumba hutumia umeme wa nje kwa madhumuni ya mapambo na usalama. Wakati unataka kununua taa kwa ajili ya taa za nje, utaona bidhaa mbalimbali, kuanzia taa zenye volteji ndogo hadi kubwa.
- Zima taa za mapambo za nje kunapopambazuka. Tumia taa zinazotumia umeme kidogo na zinazodumu kwa muda mrefu;
 - Usishike waya wa umeme ulioanguka au kuningina kwani ni hatari kwa afya yako;
 - Usikate miti karibu na mfumo wa umeme kwani miti ikuanguka mifumo hiyo inayweza kuleta athari ya umeme;
 - Toa taarifa iwapo kuna hitilafu ya umeme kuepusha hatari; na
 - Usiruhusu nyaya za umeme kukatisha juu ya paa la nyumba yako kwani kukitokea hitilafu ya umeme unaweza kusababisha ajali ya moto katika nyumba yako.

Tahadhari

- Usijenge nyumba ya makazi au bishara chini ya nyaya za umeme kwani ni hatari kwa usalama wako;
- Tumia wakandarasi waliosajiliwa na EWURA katika kuingiza mfumo wa umeme ndani ya nyumba yako ili kuwa na uhakika wa usalama wa mfumo wa umeme;
- Usishike wala kugusa waya wa umeme ulioanguka au kuning' inia;
- Usifanye kazi za ufundi wa umeme pasipo kuwa na ujuzi, tumia mafundi wenye leseni kama kuna hitilafu yoyote ya umeme katika nyumba yako;
- Usipite maeneo yaliyokatazwa wakati wa ujenzi au matengenezo ya miundombinu ya umeme yakiendelea;
- Usisimame au kufanya biashara chini ya Transfoma ya umeme kwani ikipata hitilafu yaweza kuathiri usalama wako;
- Usikate miti karibu na mfumo wa umeme unaweza kuhatarisha maisha yako, wasiliana na TANESCO kwa msaada;
- Usipande, kubeba au kuchezea waya wa muhimili wa nguzo *stay wire* kwani unaweza kunaswa na umeme na kuhatarisha usalama wa maisha yako;
- Usiwashe au kuchoma moto chini ya mifumo ya umeme au karibu na nguzo za umeme kwani utaharibu miundombinu na kuiathiri jamii ya watumiaji wa huduma hiyo; na
- Watoto wasicheze karibu na nguzo au mifumo ya umeme kuepuka madhara ya umeme.

VIDOKEZO MUHIMU KWA WATUMIAJI WA BIDHAA ZA PETROLI



Hapa kuna njia za kufanya fedha zako kuwa na thamani zaidi kwa kila lita.

- Zingatia muda wa kujaza mafuta kwenye chombo chako cha moto:**
 - Nunua au jaza mafuta katika chombo chako cha moto wakati wa asubuhi sana kipindi ardhi ikiwa bado na ubaridi. Vituo vya mafuta vina matanki ya kuhifadhiya mafuta chini ya ardhi. Ardhi inapokuwa baridi mafuta huwa mazito zaidi, wakati kunapokuwa na joto petroli hutanuka, hivyo



kununua mchana au jioni lita yako huwa si lita kamili. Katika biashara ya petroli, uzito na joto maalumu la petroli, dizeli na mafuta ya ndege, ethanol na bidhaa nyingine za petroli vina umuhimu mkubwa sana. Upandaji wa joto wa nyuzi 1 ni suala kubwa sana katika biashara hii. Lakini vituo vya huduma ya mafuta havina namna ya kufidia joto kwenye pampu.

- Hakikisha unajaza mafuta tenki lako likiwa nusu kwa kuwa kadiri unapokuwa na mafuta zaidi kwenye tenki lako, ndivyo hewa inayokaa kwenye moja ya sehemu tupu inavyokua kidogo.
 - Petroli huvukizwa haraka tofauti na unavyoweza kufikiri. Matenki yanayohifadhi petroli yana dari la ndani linaloelea. Dari hili hutumika kama kitenganishi kisicho bayana cha petroli na angahewa, hivyo hupunguza uvukizwaji.
 - Tofauti na vituo vya mafuta, baadhi ya magari yanayojazwa mafuta yana ufidiaji wa joto halisi kiasi kwamba kila lita huwa na kiasi halisi.
- Usijaze mafuta wakati gari la mafuta linamimina mafuta kwenye matenki ya kuhifadhiya ili kuepuka kupata mafuta yenye uchafu.
 - Mara nyingi petroli/dizeli hukorogwa kipindi mafuta yanapokuwa yanamiminwa. Kwahiyo kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha mafuta kuchanganyikana na uchafu ambao kwa kawaida hutuama chini ya tenki.

ii Risiti ya malipo

- Chukua risiti pindi unaponunua mafuta. Hii itakusaidia kulalamika ukipatwa na madhara yatokanayo na mafuta hayo.
- Risiti hutumika kama ushahidi wa manunuzi ya huduma kutoka kwenye kituo husika.

Jinsi ya Kuwasiliana Nasi:
Jengo la PSSSF Kamarage Ghorofa ya Kumi;
Mtaa wa Tambuka Reli; S.L.P. 772, Dodoma Tanzania,
Simu: 026 296 0096. Wavuti: www.ewuraccc.go.tz
Barua pepe: info@ewuraccc.go.tz
Tembelea mitandao yetu ya kijamii kupitia:

VIDOKEZO MUHIMU KWA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA MAJI



Kwa matumizi bora ya maji tunaweza kusaidia kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kizazi cha sasa na kijacho, kuokoa fedha na kulinda mazingira. Kumbuka kila tone lina thamani. Mambo yafuatayo ni muhimu kuyazingatia:-

- Usimwage maji chini wakati yanaweza kutumiwa kwa matumizi mengine mfano: kumwagilia mimea au bustani, au kwa ajili ya kufanyia usafi;
- Hakikisha kuwa nyumbani mwako hakuna maji yanayovuja. Nyumba nyingi zina sehemu zilizojificha zinazovuja.
 - Ili kubaini mvujo, funga mabomba yote, kisha kagua mita yako, kama mita itakua inazunguka basi jua kuna sehemu panavuja
 - Chunguza mfumo mzima wa mabomba ikiwemo mabomba ya nje na ndani kote kwa mfano, mabomba ya chooni na tanki la choo kuangalia kama kuna uvujaji lakini unaweza kuchunguza uvujaji kwa kuongeza rangi ya chakula kwenye tangi. Iwapo tangi linavuja, rangi itaonekana kwenye tundu la choo ndani ya kipindi cha dakika 30.
- Iwapo kifungua maji cha kwenye tanki la maji ya choo ambacho mara zote kinapokuwa chini huruhusu maji kuendelea kutoka kibadilishwe au kirekebishwe ili kiweze kurudi juu chenyewe kisiruhusu maji kuendelea kutoka.
 - Epuka kuvuta maji "kuflash" maliwatoni kama hakuna sababu ya kufanya hivyo;
- Unapojaza tenki la juu hakikisha unazima pampu ya maji haraka baada ya tenki hilo kujaa ili kuepusha maji kumwagika bila sababu;
- Ikiwa maji yamekatika, usiache koki ya bomba lako wazi kwa kuwa huenda maji yakaanza kutoka pasipo wewe kujua na hivyo kusababisha upotevu mwingi wa maji usio na sababu;
- Toa taarifa ya mvujo na bomba zilizopasuka kwa mtoa huduma, maji yanayopotea ni gharama za mteja;
- Kinga ndoo chini ya bomba ambalo halifungi vizuri ili kuingia maji ya ziada yanayochuruzika na unaweza kutumia maji hayo uliyokinga kwa shughuli zingine
- Badilisha vifaa vya bomba vilivyochoka/vilivyochakaa kwa kuweka vipya, usifunge mipira;



- Kwa wanaotumia bomba la mvua kwa ajili ya kuoga, fungua bomba ili uweze kuoga; fungua ili uweze kujipaka sabuni, kisha fungua tena kujisuuza;
- Wakati wa kuosha vyombo kwa mikono, jaza sinki au beseni moja kwa maji ya sabuni, suuza kwa maji yanayotoka polepole bombani; au jaza beseni jingine kwa ajili ya kusuuza
- Tupa karatasi za chooni, wadudu na uchafu mwingine kama huo kwenye sehemu ya takataka badala ya tundu la choo;
- Dhibiti vifaa vyako vya kumwagilia maji bustanini.

Vidokezo vya Huduma ya Maji kwa ujumla

- Shiriki katika masuala ya usimamiaji wa maji;
- Kuwa makini na fuata kanuni zote za kuhifadhi na kupunguza matumizi ya maji zinazotumiwa kwenye eneo lako;
- Utumiaji wa maji yasiyo safi na salama ni hatari kwa afya;
- Toa taarifa kuhusu upotevu wowote wa maji hasa utokanao na mabomba yaliyopasuka, mabomba wazi ya maji, maji yanayomwagika ovyo, visima vinavyovuja maji n.k) kwa mamlaka husika au watoa huduma za maji;
- Hamasisha mfumo wakusaidia, kuendeleza na kuboresha tabia ya uhifadhi maji miongoni mwa watoto na watu wazima;
- Saidia miradi ambayo itasababisha ongezeko la matumizi ya maji machafu kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi mengine;
- Wahamasishe marafiki na majirani zako kuwa sehemu ya jamii yenye ufahamu kuhusu masuala ya maji;
- Hifadhi maji kwa vile ni kitu sahihi kufanya hivyo. Usipoteze maji kwa sababu mtu mwingine ndiye anayelipia bili; na
- Jaribu kufanya kitu fulani kila siku ambacho kitaokoa maji. Usijali iwapo uokoaji ni mdogo kwani unaweza kuleta mabadiliko.

VIDOKEZO MUHIMU KWA MTUMIAJI WA GESI ZA KUPIKIA MAJUMBANI (LPG)



Gesi itumikayo majumbani ni zao litokanalo na kusafishwa kwa mafuta ghafi (crude oil). Huhifadhiwa kwenye mitungi. Gesi ni nishati safi na salama kwa mazingira. Mtumiaji anapaswa kuzingatia misingi ya usalama ili kujiepusha na madhara yanayoweza kujitokeza wakati wa utunzaji na utumiaji.

Vidokezo muhimu kwa watumiaji wa gesi za kupikia majumbani

Vidokezo vifuatavyo ni muhimu kuvizingatia ili kukidhi mahitaji ya afya, usalama na mazingira kwa watu na mali zao:

Usafirishaji

- Mtungi usafirishwe ukiwa umesimama wima kuepusha mtikisiko
- Uteremshwe taratibu kutoka kwenye gari au kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine kuepusha uharibifu wa mtungi

Ununuzi

- Nunua gesi iliyo kwenye mitungi ambayo ina lakiri ya kampuni husika (mfano: MIHAN GAS, ORXY, LAKE GAS, OILCOM, CAMEL OIL, MANJIS n.k)
- Pima uzito wa mtungi ili kujiridhisha na uzito wa gesi unayonunua
- Dai na tunza risiti ya manunuzi ya mtungi huo wa gesi mpaka itakapoisha

Uhifadhi/Utunzaji

- Hifadhi Mtungi:**
 - Ukiwa umesimama wima
 - Sehemu yenye hewa ya kutosha
 - Mbali na vyanzo vya moto au vitu vyenye mlipuko



- au vinavyoshika moto kwa haraka
 - Mahali ambapo si rahisi kugongwa au kuangukiwa na kitu chochote
- Mtungi tupu uhifadhiwe sehemu isiyokuwa na joto

Utumiaji

- Hakikisha mtungi na jiko vimeunganishwa vizuri na kiusalama
- Usifunge milango/madirisha wakati unatumia gesi kuruhusu hewa kuingia
- Hakikisha unatumia mpira (horse) unaotakiwa, usijikunje
- Kuwa karibu na jiko lako mara kwa mara unapopika ili kugundua kama kuna hitilafu yoyote

Tahadhari ya moto inayoweza kusababishwa na mvujo wa gesi

Mvujio wa gesi ukikutana na chanzo cha moto unaweza kusababisha moto/mlipuko wa moto. Mvujio unaweza kutokea kwenye/wakati:

- Maunganisho
- Mpira chakavu
- Kusahau kuzima kidhibiti gesi baada ya kumaliza matumizi
- Ubovu wa valvu
- Kukosea kuunganisha kidhibiti gesi "regulator"
- Watoto kuchezea stovu/mtungi

Ukigundua kuna uvujaji wa gesi chukua tahadhari zifuatazo:-

- Usiwashe jiko lako la gesi
- Zima jiko kama lilikuwa linatumika
- Fungua milango na madirisha kuruhusu hewa kuingia
- Usiwashe /usizime kifaa chochote cha umeme
- Usitumie simu ya mkononi ukiwa katika eneo hilo
- Usikague mvujo wa gesi kwa kuwasha kiberiti kwani inaweza kusababisha mlipuko
- Endapo gesi imevuja, tembea polepole (nyata) ili kusiwe na msuguno wa miguu na sakafu unaoweza kuleta mlipuko

Jinsi ya Kuwasiliana Nasi:
Jengo la PSSSF Kamarage Ghorofa ya Kumi;
Mtaa wa Tambuka Reli; S.L.P. 772, Dodoma Tanzania,
Simu: 026 296 0096. Wavuti: www.ewuraccc.go.tz
Barua pepe: info@ewuraccc.go.tz
Tembelea mitandao yetu ya kijamii kupitia: